PRESS RELEASE

PR21/256

# Bodi ya Utendaji ya IMF yaidhinisha Msaada wa Dharura wa Dola Milioni 567.25 [US$] za Kimarekani kuisaidia Tanzania kukabiliana na Janga la COVID-19

**KUTOLEWA MARA MOJA**

- Mlipuko wa COVID-19 umesababisha kuporomoka kwa sekta ya utali na kuzidisha mahitaji ya ufadhili mkubwa wa fedha kukabiliana na athari za janga hili.
- IMF imeidhinisha dola milioni 567.25 za Kimarekani za msaada wa dharura wa fedha chini ya Mradi wa Mikopo ya Haraka na Chombo cha Kufadhili kwa Haraka ili kusaidia juhudi za maafisa wa serikali kukabiliana na janga kwa kushughulikia mahitaji ya dharura ya afya, kibinadamu na kiuchumi. Rasilmali hizo zinatarajiwa kuwa na jukumu la kuchochea juhudi zao katika kukusanya msaada zaidi kutoka kwa washirika wa maendeleo.
- Maafisa wa serikali waahidi pia kuimarisha utawala bora na uwazi ili kuhakikisha kwamba rasilmali za fedha zinatumiwa vyema kukabiliana na mzozo.

**Washington DC – Septemba 7 2021:** Bodi ya Shirika la Fedha la kimataifa (IMF) imeidhinisha hii leo kutolewa kwa mkopo wa SDR milioni132.6 (dola milioni 189.08 za Kimarekani) chini ya Mradi wa Mkopo wa Haraka (RCF) Rapid Credit Facility na mkopo wa ununuzi uliyo sawa na SDR milioni 265.2 (dola milioni 378.17 za Kimarekani) chini ya Chombo cha Kufadhili kwa Haraka (RFI) Rapid Financing Instrument ikiwa jumla ya SDR milioni 397.8 sawa na (dola milioni 567.25 za Kimarekani au asili mia 100 za fungu lake). Ufadhili huu wa dharura utasaidia Tanzania kugharimia mahitaji yake ya dharura ya kuhudumia ulipaji wa madeni yake ya kimataifa kutokana na mlipuko wa janga la COVID-19.

Mtizamo wa uchumi wa Tanzania ulishuka sana kutokana na athari za janga la COVID-19 Kutokana na kuporomoka kwa utali kufuatia vizuizi vya usafiri, inaripotiwa uchumi ulishuka hadi ukuwaji wa asili mia 4.8 kwa mwaka 2020, na ukuwaji unatarajiwa kubaki dhaifu kwa mwaka 2021.

Tanzania inakabiliwa na mahitaji ya dharura ya kuhudumia ulipaji wa madeni yake kwa asili mia 1.5 ya GDP wakati wakuu wa serikali wakitekeleza mpango kabambe wa kupunguza athari za janga na kuuwezesha uchumi kuwa thabiti inapokabiliwa na kile kinacho ripotiwa kuwa ni wimbi la tatu la mambukizo ya virusi.

Kutolewa kwa mkopo chini ya RCF na mkopo wa ununuzi chini ya RFI itasaidia kugharimia mipango inayohitaji kupunguza makali ya athari za kijami na kiuchumi kutokana na janga la ugonjwa na kusaidia kuharakisha kupata msaada kutoka kwa washirika wa maendeleo.

Maafisa wa serikali wameeleza kwamba wanadhamira ya dhati kufuata sera za uchumi zinazostahiki kwa ajili ya kushugulikia athari za janga la ugonjwa na wanadhamira ya kuimarisha uratibu na uwazi ili kuhakikisha kwamba rasilmali za RCF na RFI zinatumika kupambana na janga la ugonjwa. Hatua hizi ni pamoja na kuchapisha ripoti za matumizi ya fedha za RCF na

RCI, na kufanya ukaguzi wa baada ya mzozo kuhusu matumizi yote yanayohusiana na janga la ugonjwa wa COVID.

Kufuatia majadiliano ya Bw. Bo Li, Naibu Mkurugenzi Mtendaji na Mwenyekiti, wametoa taarifa ifuatayo.

"Janga la COVID-19 limeathiri vibaya mtizamo wa uchumi jumla wa Tanzania pamoja na afya ya ustawi wa raia wake. Ukuwaji ulishuka mwaka 2020 na hautarajiwi kupanda sana katika mwaka 2021, hivyo kuongeza umaskini na atahri katika ajira. Hatari ya kuongezeka tatizo la madeni ya nje na ya umaa iliongezeka kufikia wastani hasa kutokana na athari za janga kwa biashra ya utali. Mtizamo wa uchumi jumla wa Tanzania unategemea kushughulikiwa janga hili kwa njia ya kuridhisha, lakini hatari kubwa zaidi ingali inatokana na hali ya kutokua na uhakika kuhsu jinsi janga litakavyoendelea.

"Maafisa wa serikali wanatekeleza mpango kabambe wa kukabiliana na janga—Mpango wa Tanzania wa kushughulikia masuala ya Kijamii na Kiuchumi kutokana na COVID-19 (TCRP) —kushughulikia madhara ya mshtuko wa COVID-19. Tanzania inahitaji msaada wa dharura wa kifedha ili kutekeleza mpango huo na kuepusha madhara mabaya ya kiafya, kijamii na kiuchumi kutokana na kuripotiwa wimbi la tatu la virusi. Msaada wa dharura kupitia Mradi wa Mkopo wa Haraka na Chombo cha Kufadhili kwa Haraka utachangia sana kukidhi mara moja mahitaji ya fedha kutoka nje na kusaidia kuhamasisha msaada kutoka kwa wafadhili. Kulegezwa kwa muda sera za uchumi jumla na za fedha kutapunguza atahri mbaya za janga, kufanya kampeni ya chanjo, kuongeza matumizi katika afya na huduma za kijami, na kusaidia sekta ya binafsi. Kuweka kipaumbele katika kushughulikia afya, kuimarisha uratibu na uwazi ili kuhakikisha kwamba fedha zilizopokelewa zinatumiwa katika kupambana na janga na kuripoti kwa kawaida na uwazi takwimu za maambukizo itakua muhimu kwa ufanisi wa mpango huo.

"Kudumisha uendelevu wa kifedha na deni, na kuhifadhi uendelevu wa kifedha wakati huo huo kusaidia uchumi itakua muhimu vile vile. Kufuatilia kwa karibu ustawi wa mfumo wa mabenki kutokana na kuongezeka kwa madhara kwenye sekta ya mabenki itakua ni nyeti.

"Mara mzozo utakapopungua maafisa wa serikali wana nia kama inavyostahili kuanza tena utekelezaji wa mageuzi ili kuweza kua na ukuwaji endelevu na kuwahusisha wote. Ajenda yao pana ya sera na mageuzi inajumuisha mageuzi ya mapato ya umaa ili kuepusha kutolipa kwa wakati madeni ya ndani na ziada za kodi, kuongeza msaada kwa ajili ya matumizi kwenye elimu na afya na kuimarisha mazingira ya biashara."

*Habari zaidi*

Kipimo cha kufuatilia ukopeshaji cha IMF (ombi la ugharimiaji wa dharura limeidhinishwa na Bodi ya Utendaji ya IMF)

https://www.imf.org/en/Topics/imf-and-covid19/COVID-Lending-Tracker

Kalenda ya Bodi ya Utendaji ya IMF

https://www.imf.org/external/NP/SEC/bc/eng/index.aspx